

9.0. MUUNDO WA TUME HURU YA UCHAGUZI.

15th December 2020. Chanzo cha wazo hili ni **Uchaguzi Mkuu 2020**

- 1.1. Kutakuwa na wajumbe/Makamishina 12 wa Tume Huru ya Uchaguzi ambao watatoka katika taasisi zifuatazo:
- 1.2. Wajumbe/Makamishina wanne (4) watapendekezwa na vyama vya siasa ambavyo vilishawahi kupata zaidi ya asilimia 20 kwenye matokeo ya uchaguzi mkuu wowote ndani ya miaka 15 kabla ya uchaguzi mpya. Wajumbe hao watagawanywa kwa usawa kwa vyama vitakavyokuwa na vigezo vilivyotajwa katika kifungu hiki.
- 1.3. Wajumbe/Makamishina wanne (4) watapendekezwa na vyama vya siasa ambavyo vilishawahi kupata chini ya asilimia 20 kwenye matokeo ya uchaguzi mkuu wowote ndani ya miaka 15 kabla ya uchaguzi mpya. Wajumbe hao watapendekezwa baada vikao vya viongozi wa vyama husika kukubaliana.
- 1.4. Wajumbe/Makamishina wawili (2) watapendekezwa taasisi za kidini kwa uwiano wa dini kuu mbili zitazotambulika nchini.
- 1.5. Wajumbe/Makamishina wawili (2) watapendekezwa na asasi za kiraia baada ya vikao vya pamoja na kukubaliana.
- 1.6. Wajumbe wote hawapaswi kuwa wafuasi wa vyama vya siasa au watumishi wa serikali. Kwa wale wajumbe ambao wamependekezwa na vyama vya siasa na ni wanachama watalazimika kujiuzulu uanachama wao kwa kiapo cha wakili yoyote wa mahakama kuu.
- 1.7. Kwamba baada ya kupatikana wajumbe wote 12 kutoka kwenye taasisi husika, wajumbe hao watakutana na kufanya kikao cha kupendekeza Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi miongoni mwao. Kwa lugha nyingine wajumbe hao watakuwa ndio makamishina wa uchaguzi.

1.8. Baada ya kukamilisha mchakato wa kumpata Mwenyekiti na Mkurugenzi wa tume Huru ya Uchaguzi hatua itakayofuata ni kula kiapo cha uaminifu mbele ya Jaji Mkuu kwa Mwenyekiti, Mkurugenzi na wajumbe au makamishna wote wa Tume Huru ya Uchaguzi.

1.9. Wasimamizi wa Uchaguzi ngazi majimbo ya uchaguzi.

1.10. Nafasi za Wasimamizi wa Uchaguzi ngazi ya majimbo zitatangazwa ili kuwapa nafasi watu wenye sifa kuwasilisha maombi yao kupitia ofisi ya Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi. Kikao cha Tume Huru ya Uchaguzi chini ya mwenyekiti na wajumbe kitafanya usaili wa Wasimamizi wa Uchaguzi na kuwapangia vituo vyao vya kazi.

1.11. Wasimamizi wasaidi wa Uchaguzi ngazi ya Kata.

1.12. Nafasi za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata zitatangazwa ili kuwapa nafasi watu wenye sifa kuwasilisha maombi yao kupitia ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo. Kikao cha wadau wa Uchaguzi ngazi ya jimbo kitakachoongozwa na Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo/majimbo na kujumuisha wagombea ubunge na wagombea udiwani pamoja na viongozi wa vyama vya siasa kitafanya usaili wa wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata na kuwapangia vituo vya kazi.

1.13. Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, Maafisa wa Uchaguzi na makarani waongozaji.

1.14. Nafasi za Wasimamizi wa vituo vya Kupigia pamoja na Makarani waongozaji zitatangazwa ili kuwapa nafasi waombaji kuwasilisha maombi yao kwa Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo. Kikao cha wadau wa Uchaguzi ngazi ya jimbo chini ya Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo/majimbo kitafanya usaili wa wasimamizi wa vituo vya kupigia kura na makarani waongozaji kisha kuwapangia vituo vya kazi.

1.15. Kutakuwa na maafisa wa uchaguzi ambao wataajiriwa kutokana na mahitaji ya Tume Huru ya Uchaguzi .

1.16.Muda wa Tume Huru ya Uchaguzi, Utendaji wake na Mamlaka zake.

1.17. Tume Huru ya Uchaguzi itahudumu kwa vipindi viwili vya uchaguzi na utaratibu wa muundo wa Tume Huru ya Uchaguzi utaendelea kuwa hivi hivi kama ilivyoanishwa hapo juu.

1.18. Mwenyekiti, MKurugenzi, Wajumbe/Makamishina na Wasimamizi wa Uchaguzi watakuwa waajiriwa wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mkataba wa miaka 10. Hivyo hawataruhusiwa kujihusisha na vyama vya siasa wala kuajiriwa na serikali au kuteuliwa nafasi zozote za serikali mpaka mkataba wa mika 10 utakapomalizika. Hii ni kwa ajili ya kuepusha mgongano wa kimaslahi na upendeleo.

1.19. Wasimamizi Wasaidizi ngazi ya kata, Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura na Makarani waongozaji zitakuwa ajira za muda mfupi hasa katika vipindi vya uchaguzi.

1.20. Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa shuguli zote za Uchaguzi na ndiye atakayekuwa na mamlaka ya kutangaza matokeo ya uchaguzi ngazi ya Urais kwa kila jimbo baadaye kwa ujumla wake baada ya majumuisho.

1.21. Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa shughuli zote za uchaguzi na kuwasilisha taarifa kwa Mwenyekiti kisha kuwafikishia wajumbe/Makamishina wa Uchaguzi kwenye vikao.

1.22. Makamishina wa Uchaguzi au Wajumbe watakuwa na kazi ya kupitisha kanuni, Mipango, Bajeti na kushiriki shughuli zote za uchaguzi.

1.23. Tume Huru ya Uchaguzi itakuwa huru kuanzia watumishi wake mpaka utendaji wake. Tume Huru ya Uchaguzi haitalazimika kufuata maagizo au maelekelezo yoyote kutoka mamlaka yoyote isipokuwa kama kutakuwa na maombi yaliyowasilisha mahakamani na mahakama ikaona maombi hayo ni ya msingi.

1.24. Mtumishi yoyote wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye utendaji wake ulisababisha matokeo ya Uchaguzi ngazi yoyote kutenguliwa na mahakama kwa sababu ya makosa yanayohusu upigaji na uhesabuji wa kura atafukuzwa kazi na kufunguliwa mashtaka.

1.25. Itakuwa marufuku kwa askari au afisa yoyote wa chombo cha dola kuingia ndani ya chumba cha kupigia kura bila kibali cha msimamizi wa kituo cha kupigia kura na mawakala wa vyama vya siasa.

1.26. Jeshi la polisi na vyombo vingine vya dola hawatahusika na shughuli zozote za uchaguzi zaidi ya kuweka ulinzi kwa mujibu wa kanuni zitakazowekwa na Tume wakati wa uchaguzi husika.

1.27.Kukoma Utumishi wa Tume Huru ya Uchaguzi.

1.28. Kukiuka maadili ya Utumishi na kiapo cha kazi.

1.29. Kufariki.

1.30. Kujiuzulu.


1.31. Mtumishi aliyemaliza mkataba wake anayo haki ya kuteuliwa tena na taasisi yake katika muhura unaofuata.

1.32. Kwa mtumishi yoyote wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye utumishi wake umekoma kwa sababu zilizotajwa hapo juu, basi nafasi yake itazibwa na mtu

mwingine kutoka taasisi husika kama utaratibu ulivyowekwa wa kuwapata wajumbe.

Mwisho.

*Muundo huu wa **Tume Huru ya Uchaguzi** umeandaliwa na Mdude Mpaluka Nyagali. Ni matumaini yangu kwamba kuna siku muundo huu utakuwa sheria . Na hapo utakuwa mwanzo wa wananchi kuheshimiwa na utakuwa mwisho wa wananchi kudanganywa.*

A handwritten signature in black ink, reading "Mpaluka Nyagali". The signature is written in a cursive style with a large, stylized 'N'. Below the signature is a horizontal dotted line.

Mdude Mpaluka Nyagali.